

## **Lugha ya A2 (A2-kieli) itachaguliwa katika kipindi cha 10.-21.1.2022.**

Wanafunzi wa darasa la tatu wana uwezekano wa kuchagua lugha ya kigeni ya ziada, yaani lugha ya A2 (A2-kieli). Masomo haya yataanza mwanzoni mwa darasa la nne. Mwanafunzi achague kati ya lugha zifuatazo: Kijerumani (saksa), Kifaransa (ranska), Kihispania (espanja) na Kirusi (venäjä).

Ikiwa mwanafunzi ameanza kwenye darasa la kwanza masomo ya Kijerumani, Kifaransa, Kirusi au Kifini kama lugha mama, anaanza somo la Kiingereza kwenye darasa la nne kama lugha ya A2 (A2-kieli). Kwenye somo la Kiingereza A2 malengo yaleyale kama katika somo la lugha ya Kiingereza A1 yatafikiwa mpaka mwishoni mwa darasa la 9.

Lugha ya A2 (A2-kieli) itachaguliwa katika kipindi cha 10.-21.1.2022. Walezi watatumwa mapema ujumbe wa Wilma wenyenye maelezo juu ya kuchagua lugha. Taarifa juu ya vikundi vya lugha vitatolewa tarehe 2.2.2022. Kikundi cha lugha kitaanzishwa ikiwa wanafunzi angalau 12 wanachagua lugha ileile ya A2 kama chaguo la kwanza au la pili. Hata uchaguzi wa lugha ya pili hauwezi kubadilishwa baadaye.

Chaguo la lugha ya A2 ni la hiari lakini ikiwa mwanafunzi amechagua lugha fulani inambidi kuisoma mpaka mwishoni mwa darasa la 9. Lugha ya A2 ni somo mojawapo kati ya masomo yote ambayo wanafunzi wanayachagua katika shule ya msingi kiwango cha juu.

Wanafunzi wamepewa maelezo juu ya lugha za A2 katika muhula wa vuli (syyslukukausi). Katika shule chache maelezo haya bado yataendelea mwezi wa kwanza. Unaweza kusoma kuhusu chaguo la lugha katika kiuongo hiki: <https://peda.net/jyvaskyla/kieku/a2-kieliryhmat>

Sehemu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara juu ya chaguo la lugha inapatikana katika kiungo hiki: Lisätietoja kielivalinnasta.

### **Vikao kwa wazazi kwa kupitia mtandao kuhusu chaguo la lugha ya A2**

Vikao viwili vyenye taarifa aina moja vitapangwa mwezi wa kwanza kwa wazazi kuhusu chaguo la lugha ya A2. Vikao hivi vitapangwa kwa kupitia Teams kwenye mtandao (Teams-yhteys) tarehe zifuatizo:

**11.1.2022 18.00-19.30**

[https://teams.microsoft.com/meetingOptions/?organizerId=2ed4380d-cd72-4893-bc39-64e39f754158&tenantId=fc34d05c-a2f2-4ac2-89c5-b44f3a9f451c&threadId=19\\_meeting\\_NjIyMDk1ZWQtZTFjYS00NDU1LTk3ZjItYjEzNDY3MmI2Mzc5@thread.v2&messageId=0&language=fi-FI](https://teams.microsoft.com/meetingOptions/?organizerId=2ed4380d-cd72-4893-bc39-64e39f754158&tenantId=fc34d05c-a2f2-4ac2-89c5-b44f3a9f451c&threadId=19_meeting_NjIyMDk1ZWQtZTFjYS00NDU1LTk3ZjItYjEzNDY3MmI2Mzc5@thread.v2&messageId=0&language=fi-FI)

**18.1.2022 18.00-19.30**

[https://teams.microsoft.com/meetingOptions/?organizerId=2ed4380d-cd72-4893-bc39-64e39f754158&tenantId=fc34d05c-a2f2-4ac2-89c5-b44f3a9f451c&threadId=19\\_meeting\\_MjUyYjQ4YTUtNDI0YS00ODEyLWE5ZTYtYjFmYzI5YjkwOGRh@thread.v2&messageId=0&language=fi-FI](https://teams.microsoft.com/meetingOptions/?organizerId=2ed4380d-cd72-4893-bc39-64e39f754158&tenantId=fc34d05c-a2f2-4ac2-89c5-b44f3a9f451c&threadId=19_meeting_MjUyYjQ4YTUtNDI0YS00ODEyLWE5ZTYtYjFmYzI5YjkwOGRh@thread.v2&messageId=0&language=fi-FI)

Taarifa nyingine kutoka kwa Mkuu wa Shule, walimu wa lugha na Mkuu wa Huduma ya Mafundisho kwa vikundi vya lugha na utamaduni Pia Bärlund (040-5455 257, pia.barlund@jyvaskyla.fi ).